# MUHTASARI WA SERA

## MATUMIZI YA TAKWIMU ZA MSINGI ZA KIDEMOGRAFIA, KIJAMII NA KIUCHUMI KWA AJILI YA SERA NA MIPANGO YA MAENDELEO YENYE UFANISI TANZANIA

2024

# MUHTASARI WA SERA

# MATUMIZI YA TAKWIMU ZA MSINGI ZA KIDEMOGRAFIA, KIJAMII NA KIUCHUMI KWA AJILI YA SERA NA MIPANGO YA MAENDELEO YENYE UFANISI TANZANIA

**2024**

## 1.0 Usuli

Ripoti ya Taarifa za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi ya Mwaka 2022 inatoa uchambuzi mfupi wa viashiria muhimu vitokanavyo na taarifa zilizokusanywa katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 (SWM 2022). Viashiria hivyo vitatumika katika kutunga sera, kuandaa mipango, kupima mafanikio na changamoto za utekelezaji wa programu za maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Taarifa ya Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi ina viashiria vya ongezeko la idadi ya watu; mgawanyo wa watu kwa jinsi na umri; muundo wa kaya, hali ya ndoa; vitambulisho vya kitaifa na uraia; uhai wa wazazi; elimu; kujua kusoma, kuandika na kuhesabu; ajira na shughuli za kiuchumi; na hali ya ulemavu. Viashiria vingine ni umiliki wa ardhi; hali ya makazi; umiliki wa vifaa na huduma katika makazi; upatikanaji na matumizi ya vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na udhibiti wa mazingira.


Taarifa hii ya kisera inaonesha umuhimu wa matumizi ya takwimu zilizopo kwenye Ripoti ya Taarifa za Msingi za Kidemografia, Kijamii na Kiuchumi nchini kwa ajili ya kutoa taarifa za kisera, programu za maendeleo na uwekezaji zitakazowezesha maendeleo endelevu na kuboresha maisha ya Watanzania wote. Wanufaika wakubwa wa taarifa hizi ni watunga sera, maafisa mipango na wawekezaji wa ndani na nje pamoja na wadau wengine.

## 2.0 Idadi, Ongezeko na Mgawanyo wa Watu

Kiashiria cha kwanza cha kidemografia kitokanacho na sensa ya watu na makazi ni idadi ya watu. Idadi ya watu ni kiashiria muhimu kwa ajili kupanga, kufuatilia na kukadiria mahitaji ya rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi yoyote. Ongezeko la idadi ya watu husababisha ongezeko la mahitaji kwa ajili ya huduma za kijamii kama vile elimu, afya, miundombinu, na kupitia upya mipaka ya maeneo ya kiutawala, ukuaji wa miji na matumizi ya ardhi.

Ongezeko la idadi ya watu linaweza kusababisha kuongezeka kwa ukosefu wa ajira, upungufu wa rasilimali za kukidhi mahitaji ya msingi ya kijamii na kiuchumi, uchafuzi wa mazingira, hasa uzalishaji wa gesi ya ukaa, uharibifu wa ardhi na vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za kibinadamu.

Kielelezo Na.1: Ongezeko la Idadi ya Watu Tanzania,1967 – 2022 SWM




**Matokeo Muhimu**

Idadi ya watu Tanzania inaongezeka kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka.

**Tafsiri ya Kisera**

i. Idadi ya watu Tanzania imekuwa ikiongezeka kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka kati ya mwaka 2012 na 2022. Hii ni sawa na ongezeko la watu milioni 16.8 ambayo ni sawa na asilimia 37.4 kwa kipindi cha miaka kumi. Kwa kasi hii ya ongezeko, idadi ya watu Tanzania inategemewa kuongezeka mara mbili katika kipindi cha miaka 22 ijayo. Hii ina maana kuwa, ifikapo mwaka 2044, Tanzania inategemewa kuwa na watu milioni 123.4;

ii. Ongezeko la idadi ya watu, likisimamiwa vizuri linaweza kuwa fursa ya kiuchumi kutokana na uboreshaji wa akiba katika kaya ambazo zinaweza kuchochea uwekezaji na hatimaye kupunguza umaskini. Ongezeko hili linachangia kuongezeka kwa nguvu kazi na ushiriki katika uzalishaji wa bidhaa na huduma na hivyo kupelekea ushindani wa kibiashara; kuongezeka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja na hisa za soko la bidhaa ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya kijamii na kiuchumi;

iii. Kwa upande mwingine, kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu inaweza kusababisha yafuatayo:-

   a) Ukosefu wa ajira, uchafuzi wa mazingira hasa utoaji wa gesi ya ukaa, uharibifu wa ardhi na vyanzo vya maji unaotokana na shughuli za kibinadamu;
   b) Ongezeko la mahitaji kwa ajili ya huduma za kijamii kama vile elimu, maji, afya, miundombinu ya usafirishaji, nishati na nyumba, hali ambayo husababisha ongezeko la bajeti za Serikali na hivyo kupunguza kasi ya upatikanaji wa mitaji na akiba kwa uwekezaji wenye tija; na
   c) Mahitaji ya kupitia upya maeneo ya kiutawala, ukuaji holela wa miji na upungufu wa ardhi.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali ione uwezekano wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Mwaka 2006 ambayo lengo lake kuu lilikuwa ni kujumuisha masuala ya idadi ya watu katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa;

ii. Serikali na wadau wengine kuendelea na usimamizi wa mikakati inayowawezesha wavulana na wasichana kupata elimu ya msingi hadi sekondari ili kutokomeza ndoa za utotoni kwa wasichana;

iii. Wizara za sekta husika, ziendelee kuimarisha utoaji wa huduma za uzazi wa mpango na kuhakikisha kuwa zinawafikia wanawake walio katika umri wa kuzaa; na

iv. Serikali iendelee kuimarisha programu zinazohusiana na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ili kuendelea kuwajengea uwezo wa kutoa maamuzi sahihi kuhusu afya ya uzazi.

***Kuongezeka mara mbili kwa idadi ya watu ya sasa kufikia watu milioni 123.4 ifikapo mwaka 2044 ni: -***

- ***Ishara ya kuwa na hatua za kimkakati kwa upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya shughuli za kijamii, kiuchumi na mazingira;***
- ***Kiashiria muhimu kwa maamuzi ya kimkakati kuhusu uwekezaji na biashara katika Ukanda wa Mashariki mwa Afrika.***

## 3.0 Taarifa za Umri na Jinsi

Umri na jinsi ni taarifa muhimu za kidemografia za idadi ya watu. Ni taarifa muhimu katika uchambuzi wa mienendo ya idadi ya watu, uchambuzi wa kidemografia, majukumu na wajibu katika mchakato wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Umri ni taarifa muhimu katika kupanga na kufanya maamuzi sahihi katika utawala wa umma kwa makundi mbalimbali ya watu. Kwa mfano, umri unatumika kwenye utoaji wa huduma za afya, chakula na makazi, ushiriki wa nguvu kazi, uandikishwaji wa watoto shuleni na katika kufanya makisio ya idadi ya watu.

**Matokeo Muhimu**

i Mgawanyo wa idadi ya watu kwa umri nchini Tanzania, unaonesha uwepo wa asilimia kubwa ya watoto; ambapo asilimia 42.8 ya watu wote wana umri chini ya miaka 15;

ii Takribani asilimia sita ya watu wote Tanzania wana umri wa miaka 60 au zaidi; na

iii Uwiano wa utegemezi wa umri Tanzania ni wategemezi 87 kwa kila watu 100 wenye umri wa kufanya kazi.


**Tafsiri ya Kisera**

i. Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watu wenye umri mdogo Tanzania ni matokeo ya idadi kubwa ya watu inatokana na viwango vya juu vya uzazi miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kuzaa na viwango vya juu vya vifo kadiri umri unavyoongezeka. Uwepo wa idadi ya watu wengi wenye umri mdogo una umuhimu mkubwa kisera kwa sekta mbalimbali, zikiwemo sekta za elimu, ajira, afya na maendeleo ya jamii. Kuelewa tafsiri hizi za kisera ni muhimu kwa watunga sera katika kufanya maamuzi sahihi na kutekeleza mikakati madhubuti ili kunufaika na fursa ya kuwa na idadi kubwa ya vijana na kuhakikisha kuwa mchango wao (demographic dividend) unakuwa na manufaa kwenye mipango ya maendeleo ya kitaifa ya muda wa kati na mrefu.

ii. Ongezeko la idadi ya wazee unaashiria kuongezeka kwa mahitaji ya hifadhi ya jamii kwa ajili yao; na

iii. Uwiano mkubwa wa umri tegemezi unaongeza mahitaji ya huduma za jamii za muda mrefu; mahitaji makubwa ya fedha za umma kugharamia huduma hizo na hupunguza tija katika uzalishaji.

**Kielelezo Na. 2: Mgawanyo wa Watu katika Makundi ya Umri wa Miaka Mitano; Tanzania, SWM 2022**




## Mapendekezo ya Hatua za Kisera

i. Serikali iendelee kuimarisha utoaji wa huduma bora za maendeleo ya awali ya mtoto na elimu, kuandaa mifumo madhubuti ya elimu ya msingi na sekondari ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata fursa ya kujifunza na kujiendeleza kikamilifu kadri ya uwezo wao;

ii. Serikali iendelee kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya elimu, afya, lishe, usalama, hifadhi na ulinzi wa jamii kama inavyoelekezwa katika sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sheria ya Watoto ya Zanzibar Namba 6 ya mwaka 2011;

iii. Mchakato unaoendelea wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050 pamoja na mipango yake ya muda wa kati na mrefu uzingatie mustakabali wa vijana na wazee; na
iv. Serikali ikishirikiana na wadau iangalie uwezekano wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Wazee (2003) inayotambua kuwa wazee ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa, utengaji wa rasilimali za kutosha, ushirikishwaji katika kutoa maamuzi, shughuli za kujiongezea kipato na upatikanaji wa ulinzi wa kisheria.

***Tanzania inaweza kunufaika na idadi kubwa ya vijana ikiwekeza katika mtaji watu na viwanda***

## 4.0 Kaya Binafsi

Tanzania ina jumla ya kaya binafsi 14,152,803, kati ya hizo kaya 8,547,333 (60.4%) zipo vijijini na kaya 5,605,470 (39.6%) zipo mjini. Kaya zinazoongozwa na wanawake zimeongezeka kutoka asilimia 33.5 mwaka 2012 hadi asilimia 35.9 mwaka 2022.


**Matokeo Muhimu**

Takribani asilimia 36 ya kaya binafsi zote nchini zinaongozwa na wanawake.

**Tafsiri ya Kisera**

Ongezeko la kaya zinazoongozwa na wanawake kwa sehemu kubwa limetokana na mabadiliko ya mienendo ya kiuchumi na kijamii kama vile vifo, kutengana au kuachana, ukatili wa kijinsia, umaskini na uhamaji wa vijijini kwenda mjini. Sababu hizi kwa kiasi kikubwa huathiri zaidi wanawake kiuchumi, kisaikolojia na kihisia.

**Kielelzo Na. 3: Asilimia ya Kaya Zinazoongozwa na Wanawake kwa Eneo; Tanzania, 2012 – SWM 2022**




## Mapendekezo ya Hatua za Kisera

i. Serikali na wadau iendelee kuimarisha mipango ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, kuendesha kampeni za elimu na uhamasishaji pamoja na kutoa fursa sawa za kiuchumi na kijamii kwa wote; na

ii. Serikali na wadau waimarishe utekelezaji wa sera na sheria ili kuhakikisha usawa wa jinsia na kuzuia unyanyasaji wa kijinsia na mgawanyo sawa wa mali za wanandoa

## 5.0 Hali ya Ndoa

Taarifa kuhusu hali ya ndoa husaidia serikali na watumiaji wengine kuelewa mienendo ya hali ya ndoa, kuainisha mahitaji ya baadaye ya programu ambazo zina manufaa kwa wanandoa na zinazopima athari za sera na mipango inayozingatia ustawi wa familia, ikiwa ni pamoja na mipango ya msaada wa kifedha. Wastani wa umri wa kuoa/kuolewa mara ya kwanza Tanzania umekuwa ukiongezeka. Wastani wa umri wa kuolewa umeongezeka kutoka miaka 21.1 mwaka 2002 hadi miaka 22.3 mwaka 2022. Matokeo haya yanaonesha kuwa sera za Serikali kuhusu elimu zimeanza kuonesha ishara chanya. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa chini ya asilimia moja ya wasichana wenye umri wa miaka 10 - 14 na asilimia 16.5 ya wale wenye umri wa miaka 15 - 19 wameolewa. Serikali duniani kote zimeahidi kutokomeza ndoa za utotoni ifikapo mwaka 2030 kupitia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

**Matokeo Muhimu**

i Asilimia 1.5 ya idadi ya watu walioa/waliolewa wakiwa na umri mdogo (miaka 10 - 14);

ii Wastani wa umri wa kuoa/kuolewa kwa mara ya kwanza ni miaka 22 kwa wanawake na kwa wanaume ni miaka 26;

iii Asilimia 3.7 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wametalikiana; na

iv Asilimia 4.9 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi ni wajane.

**Tafsiri ya Kisera**

i Ndoa za utotoni zina madhara ya kudumu kwenye maisha kama vile kuongezeka kwa unyanyasaji, mimba za utotoni, kuathirika kiafya, kukosekana kwa fursa kama vile elimu, shughuli za kiuchumi pamoja na athari nyingine kama za kisaikolojia;

ii Kuongezeka kwa talaka na ujane kunaweza kuleta mabadiliko ya malezi kwenye familia, ambayo yanaweza kusababisha malezi yasiyo na usawa kwa watoto kwa kuwa na mzazi mmoja. Hali hii mara nyingi hupelekea mtoto kukosa huduma za mahitaji ya msingi ikiwa ni pamoja na elimu bora na afya.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i Serikali na wadau wengine waendelee kujumuisha afua za uzuiaji ndoa za utotoni katika elimu ya mtoto wa kike;

ii Serikali na wadau wengine waendelee kuhamasisha wananchi juu ya athari za ndoa za utotoni; na

iii Serikali, Mashirika ya Dini na washirika wengine wanapaswa kuendelea kuimarisha maadili kwenye familia.

***Sera za elimu msingi bila malipo na muda mrefu masomoni zimepelekea kupungua kwa ndoa za utotoni***

## 6.0 Nyaraka za Utambulisho


Hati ya utambulisho ni hati yoyote rasmi ambayo hutumiwa kuthibitisha utambulisho wa mtu. Nyaraka za utambulisho zilizotumika katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ni Vyeti vya Kuzaliwa na Tangazo la Kizazi, Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Leseni za Udereva na Kitambulisho cha Mpiga Kura. Nyaraka nyingine za utambulisho ni Pasi ya Kusafiria, Bima ya Afya ya Taifa/Jamii na kadi nyingine za bima ya afya na Kadi ya Matibabu kwa Wazee.

**Matokeo Muhimu**

**a). Asilimia 67.1 ya watu hawana vyeti vya kuzaliwa wala tangazo la kizazi;**

Cheti cha kuzaliwa ni nyaraka ya msingi ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa mtoto. Inawezesha upatikanaji wa huduma za kijamii kama vile mahitaji ya afya na kusajiliwa shuleni. Vilevile ni hati muhimu kwa watoto chini ya miaka 18 wakati wa kuomba kitambulisho cha kitaifa, usajili wa wapiga kura na leseni ya kuendesha gari. Vile vile husaidia kuunganisha mifumo ya taarifa ya KanziData za kitaifa, masuala ya usalama wa taifa na utekelezaji wa sheria.

**Kielelezo Na. 5: Hali ya Cheti na Taarifa ya Kuzaliwa; Tanzania, SWM 2022**




## Tafsiri ya Kisera


i Idadi kubwa ya Watanzania hawana usajili wa kuzaliwa jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo (Kifungu 108, Toleo la 2002), inayoeleza kuwa mtoto anatakiwa kusajiliwa ndani ya siku 90 baada ya tukio la kuzaliwa. Hii ina maana kuwa serikali haiwezi kupanga ipasavyo mahitaji ya baadaye ya watoto. Katika ngazi ya mtu binafsi, cheti cha kuzaliwa ni hitaji la msingi la kupata huduma kama vile elimu, afya na wakati wa kuomba kitambulisho cha taifa;

ii Usajili wa kuzaliwa hutoa takwimu zinazohitajika na za karibuni zaidi za idadi ya watu ambazo ni muhimu kwa uundaji wa sera na mipango ya maendeleo. Bila usajili sahihi wa kuzaliwa, Serikali na wadau hawataweza kupanga mahitaji ya baadaye na ugawaji wa rasilimali kwa ufanisi.

## Mapendekezo ya Hatua za Kisera

i. Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika na usajili wa matukio ya Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka; na
ii. Serikali iendelee kuimarisha mfumo wa takwimu za mara kwa mara ikiwa ni pamoja na usajili wa matukio muhimu ili kukamilisha takwimu za sensa kuhusu taarifa za idadi ya watu.

**Kielelezo Na. 6: Asilimia ya Idadi ya Watu Wenye Umri wa Miaka 18 na Zaidi Walio na Kitambulisho cha Taifa; Tanzania, SWM 2022.**




**Tafsiri ya Kisera**

i. Kiwango cha ukosefu wa ajira cha asilimia 7.8 Tanzania ni cha wastani. Hii inaashiria hali nzuri ya uchumi wenye uwiano kati ya upatikanaji na mahitaji ya nguvu kazi. Ukosefu wa ajira wa wastani unaweza kushawishi waajiri kutoa maslahi bora ili kuvutia wafanyakazi;

ii. Kiwango cha wastani cha ukosefu wa ajira kinaweza kusababisha kupungua kwa matumizi ya walaji ambayo huathiri uchumi na hivyo kushuka kwa kiwango cha ubora wa maisha; na

iii. Kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira pia kinaweza kupelekea ongezeko la vitendo vya uhalifu, kukosekana kwa amani, ugumu wa maisha, kutengwa na kutojiamini.


**Mapendekezo ya hatua za Kisera**

i. Serikali inapaswa kuweka/kuhakikisha mazingira wezeshi ya kiuchumi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi katika maeneo yenye fursa za kutoa ajira mfano viwanda vya kutengeneza bidhaa;
ii. Serikali kuimarisha mazingira wezeshi, kukuza na kuvutia sekta binafsi na wadau wengine wa ajira kuelekeza uwekezaji kwenye sekta zenye kuajiri watu wengi;
iii. Taasisi za Serikali, taasisi za elimu ya juu na wadau wengine wa ajira waimarishe tafiti kuhusu ujuzi katika soko la ajira ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa katika ajira;
iv. Wizara za kisekta na wadau wa ajira kuongeza upatikanaji wa elimu na mafunzo ya amali, kukuza ujasiriamali na kujiajiri, pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya waajiri, wanaotafuta ajira, na taasisi za mafunzo; na
v. Wizara yenye dhamana ya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira zinazotosheleza mahitaji ya mipango na maamuzi.

**b) Kiwango cha Ushiriki wa Nguvu kazi kwa Tanzania ni Asilimia 77.7**

Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi ni kipimo cha uwiano wa idadi ya watu wenye umri wa kufanya kazi nchini ambao wanajihusisha kikamilifu katika soko la ajira, ama kwa kufanya kazi au kutafuta kazi. Kiwango hicho kinatoa mwelekeo wa ukubwa wa upatikanaji wa nguvu kazi inayojihusisha na uzalishaji wa bidhaa na huduma, ikilinganishwa na idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi.

**Kielelezo Na. 11: Kiwango cha Ushiriki wa Nguvu Kazi kwa Jinsi; Tanzania, 2022 SWM**




i. Watu wengi hawana bima ya afya ikimaanisha kuwa watahitaji kutumia rasilimali nyingi (ambazo huenda hawatakuwa nazo wakati zikihitajika) kupata huduma za afya. Sheria ya Bima ya Afya kwa wote iliyopitishwa mwaka 2023 ni uamuzi sahihi na wa ujasiri wa kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma bora za afya;
ii. Ni asilimia 1.2 tu ya idadi ya watu wana bima kupitia kampuni binafsi za bima ya afya.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali iendelee kufanya kampeni ya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria ya Bima za Afya (Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Tanzania ya mwaka 2023 na Sheria ya Mfuko wa Huduma ya Afya Zanzibar ya mwaka 2023) ili kukuza upatikanaji wa huduma ya afya kupitia utaratibu wa malipo ya kabla; na
ii. Wizara ya Kisekta kuzihimiza kampuni binafsi za bima ya afya kupitia upya sera zao ili kuvutia wanachama wengi zaidi.


***Hali ya Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa Tanzania bado upo chini, juhudi zaidi zinahitajika***

## 7.0 Uhai wa Wazazi na Uyatima

Taarifa kuhusu uhai wa wazazi husaidia kubaini kiwango cha uyatima katika jamii na kuwezesha kufanya maamuzi sahihi. Kifo cha wazazi kina athari kubwa kwa ustawi na maisha ya watoto wadogo, hasa wale walio chini ya miaka mitano.

Watoto wanaopoteza mzazi mmoja au wote wawili wanakosa mapenzi na huduma kutoka kwa mama na baba. Wanakabiliwa na mapambano ya kujikimu wenyewe na kujenga upya maisha yao bila msaada wa mzazi mmoja au wote wawili. Hali hii huwafanya kuwa katika mazingira magumu kihisia, kisaikolojia, kijamii na kiuchumi kwani wanajikuta wakikosa mahitaji ya maisha kama vile chakula, huduma za afya na elimu. Watoto yatima ambao wamepoteza wazazi wote wawili wakati mwingine wamekuwa wakuu wa kaya ambapo aliye mkubwa huchukua majukumu ya baba na mama kuwatunza ndugu zake.

**Kielelezo Na. 8: Hali ya Uyatima; Tanzania, SWM 2022**




**Matokeo Muhimu**

Asilimia 10.4 ya watoto Tanzania ni yatima (asilimia 7.0 mzazi mmoja amefariki na asilimia 3.4 wazazi wote wawili wamefariki).

**Tafsiri ya Kisera**

i. Uyatima unaweza kusababisha ongezeko la watoto wa mitaani, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya kaya zinazoongozwa na watoto ambazo zinaweza kuongeza umaskini wa watoto, kuongeza mateso, magonjwa, unyanyasaji wa kijamii na ukosefu wa huduma za msingi; na
ii. Ongezeko la watoto yatima (7.7% mwaka 2012 hadi asilimia 10.4 mwaka 2022) limesababisha kuongezeka kwa gharama za huduma kwa familia, jamii na serikali.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iendelee kuweka utaratibu utaopunguza madhara kwa watoto yatima ikiwemo hatua zinazohamasisha na kusaidia jamii kutoa huduma na matunzo;
ii. Serikali kwa kushirikiana na washirika wengine iendelee kuimarisha utaratibu wa kutambua walengwa kwenye familia zenye uhitaji;
iii. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iendelee kutoa fursa za elimu, afya na huduma nyingine kwa watoto yatima; na
iv. Serikali na wadau waendeleze utaratibu wa kuwafikishia fedha kaya zilizo katika mazingira magumu kama ule wa *Productive Social Security Nets* (PSSN) chini ya TASAF.


***Uyatima nchini Tanzania umeongezeka; Hatua za kuupunguza zinahitajika haraka***

## 8.0 Elimu na Hali ya Kujua Kusoma na Kuandika

Elimu ni moja ya mambo muhimu sana katika maendeleo ya jamii. Elimu inahusishwa sana na vigezo mbalimbali vya kijamii na kiuchumi, ikiwa ni pamoja na mapato na uzazi. Taarifa kuhusu elimu zimechambuliwa kwa kutumia hali ya kujua kusoma na kuandika, kuhesabu, mahudhurio shuleni, uandikishwaji, utoro shuleni na kiwango cha juu cha elimu kilichofikiwa.

Serikali, jumuiya za kikanda na kimataifa zimekuwa zikishughulika na tatizo la kutojua kusoma na kuandika kupitia mipango mbalimbali kama vile Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDPIII), Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

**Kielelezo Na. 9: Asilimia ya Watu Wenye Umri wa Miaka Mitano na zaidi Wanaojua Kusoma na Kuandika; Tanzania, 2022 SWM**




**Matokeo Muhimu**

a) Asilimia 79.1 ya watu wenye umri wa miaka mitano na zaidi wanajua kusoma na kuandika.

b) Asilimia 83.0 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanajua kusoma na kuandika.

**Tafsiri ya Kisera**

i. Nchi imepata mafanikio makubwa kuelekea kutokomeza tatizo la kutojua kusoma na kuandika ambapo itawezesha kupunguza umaskini, kuongeza ushiriki katika soko la ajira na kupelekea matokeo chanya kwa afya na maendeleo endelevu; na

ii. Kiwango cha juu cha kusoma na kuandika kinahusishwa na jamii yenye afya bora, kupungua kwa vitendo vya uhalifu, ukuaji mkubwa wa uchumi na ongezeko la ajira.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i Serikali na wadau waendelee kutenga rasilimali ili kutokomeza kabisa kutojua kusoma na kuandika kupitia mageuzi ya elimu na ushirikishwaji wa jamii;

ii Wizara za Kisekta na Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE) kuhakikisha kuwa mipango ya kutokomeza kutokujua kusoma na kuandika ni endelevu; na

iii Serikali na washirika wengine waimarishe mikakati ya kuyafikia maene yenye viwango vya chini vya kujua kusoma na kuandika ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu na maeneo yasiyofikiwa na huduma kirahisi.

c) Kiwango halisi cha uandikishwaji (NER) kwa watoto wenye umri wa miaka 7-13, kwenye shule za msingi ni asilimia 83.3; na

d) Kiwango cha jumla cha uandikishwaji (GER) kati ya watoto wenye umri wa miaka 7-13, kwa shule za msingi ni asilimia 123.2.

**Tafsiri ya Kisera**

i. Kuongezeka kwa uandikishwaji katika shule za msingi kunapelekea kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali zaidi ikiwa ni pamoja na ruzuku ya uendeshaji wa shule, miundombinu ya shule, rasilimali watu na fedha, pamoja na vifaa vingine; na

ii. Ongezeko la kiwango cha uandikishwaji wa jumla (GER) ni matokeo ya Serikali kuruhusu watoto wenye umri mkubwa kuandikishwa shuleni na hivyo kusababisha ongezeko la uandikishwaji wa jumla kuwa (GER) kuwa zaidi ya 100.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali na wadau kupanua na kuongeza miundombinu ya elimu na rasilimali watu ili kuhudumia ongezeko la uandikishwaji katika ngazi ya shule za msingi; na

ii. Wizara za kisekta na Asasi zisizo za Serikali kuimarisha mipango katika ngazi ya sekondari, vyuo vikuu na vya kati ili kukidhi ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa katika ngazi ya msingi.

Kiwango cha kujua kusoma na kuandika na uandikishwaji kimeongezeka nchini Tanzania katika kipindi cha muongo mmoja, kukiwa na tofauti kati ya mikoa

## 9.0 Ajira na Shughuli za Kiuchumi


Takwimu za ajira na shughuli za kiuchumi ni nyenzo muhimu katika kupanga sera na programu zinazohusiana na masuala ya kazi. Takwimu hizi zinatoa ukubwa na muundo wa idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi na mgawanyo wake kulingana na shughuli kuu, sekta na hali ya ajira. Taarifa zinazotokana na Sensa ni muhimu katika kuweka takwimu za msingi kwa ajili ya kuchukua hatua zinazofaa ili kuimarisha ushiriki wa nguvu kazi.

**Matokeo Muhimu**

a) **Kiwango cha Ukosefu wa Ajira ni Asilimia 7.8**

Ukosefu wa ajira una athari kubwa kwa mtu binafsi na familia. Ukosefu wa ajira husababisha ugumu wa maisha kutokana na ukosefu wa fedha, vile vile watu wasio na ajira wanaweza kuhisi kutengwa na jamii na kukosa kujiamini. Asilimia 7.8 inatokana na tafsiri wa Kimataifa ya ukosefu wa ajira (relaxed international definition of unemployment).

**Kielelezo Na.10: Kiwango cha Ukosefu wa Ajira kwa Watu wenye wa Miaka 10 na zaidi kwa Jinsi; Tanzania, 2022 SWM**



**Tafsiri ya Kisera**

i. Kiwango cha ukosefu wa ajira cha asilimia 7.8 Tanzania ni cha wastani. Hii inaashiria hali nzuri ya uchumi wenye uwiano kati ya upatikanaji na mahitaji ya nguu kazi. Ukosefu wa ajira wa wastani unashawishi waajiri kutoa maslahi bora ili kuvutia wafanyakazi;
ii. Kiwango cha ukosefu wa ajira cha wastani husababisha kupungua kwa matumizi ya walaji ambayo huathiri uchumi na hivyo kushuka kwa kiwango cha ubora wa maisha; na
iii. Kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira pia kinaweza kupelekea ongezeko la viwango vya uhalifu, kukosekana kwa amani, ugumu wa maisha, kutengwa na kutojiamini.

**Mapendekezo ya hatua za Kisera**


i. Serikali inapaswa kuweka/kuhakikisha mazingira wezeshi ya kiuchumi ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi katika maeneo yenye fursa za kutoa ajira mfano viwanda vya kutengeneza bidhaa;
ii. Serikali kuimarisha mazingira wezeshi, kukuza na kuvutia sekta binafsi na wadau wengine wa ajira kuelekeza uwekezaji kwenye sekta zenye kuajiri watu wengi;
iii. Taasisi za Serikali, taasisi za elimu ya juu na wadau wengine wa ajira waimarishe tafiti kuhusu ujuzi katika soko la ajira ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa katika ajira;
iv. Wizara za kisekta na wadau wa ajira kuongeza upatikanaji wa elimu na mafunzo ya amali, kukuza ujasiriamali na kujiajiri, pamoja na kuimarisha uhusiano kati ya waajiri, wanaotafuta ajira, na taasisi za mafunzo; na
v. Wizara yenye dhamana ya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira zinazotosheleza mahitaji ya mipango na maamuzi.

**b) Kiwango cha Ushiriki wa Nguvu kazi kwa Tanzania ni Asilimia 77.7**

Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi ni kipimo cha uwiano wa idadi ya watu wenye umri wa kufanya kazi nchini ambao wanajihusisha kikamilifu katika soko la ajira, ama kwa

kufanya kazi au kutafuta kazi. Kiwango hicho kinatoa mwelekeo wa ukubwa wa upatikanaji wa nguvu kazi inayojihusisha na uzalishaji wa bidhaa na huduma, ikilinganishwa na idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi.

**Kielelezo Na. 11: Kiwango cha Ushiriki wa Nguvu Kazi kwa Jinsi; Tanzania, 2022 SWM**




**Tafsiri ya Kisera**

i. Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi cha asilimia 77.7 ni cha wastani ambacho kinamaanisha kuwa uchumi uko imara. Kiwango hiki, pia kinaashiria kiwango cha wastani cha ukosefu wa ajira;

ii. Kiwango kikubwa cha ushiriki wa nguvu kazi kinamaanisha kuwepo kwa kiwango kikubwa cha utayari wa watu kupenda kufanya kazi;

iii. Taarifa za ushiriki wa nguvu kazi ni muhimu kwa uandaaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera ya ajira ili kuelewa tabia ya soko la ajira kwa makundi tofauti ya watu; na

iv. Taarifa ya ushiriki wa nguvu kazi huwawezesha watunga sera na watoa elimu ya ujuzi kufanya mapitio ya mitaala na kutenga rasilimali muhimu kwa ajili ya ujuzi unaotokana na mahitaji ya soko la ajira.

**Mapendekezo ya hatua za Kisera**

i. Serikali na wadau wengine kuchukua hatua za makusudi kuwawezesha vijana walio tayari na walio katika soko la ajira kwa kuimarisha na kuanzisha miradi ya mikopo na ujuzi mwingine muhimu ili kuwaweka tayari kushiriki katika uchumi; na
ii. Wizara za kisekta na wadau wengine kuimarisha mikakati na mipango mbalimbali itakayohakikisha shughuli za kiuchumi kama kilimo zinafanyika kwa mwaka mzima ili nguvu kazi inayofanya kazi kwa msimu iweze kushiriki katika uzalishaji kwa mwaka mzima.

## 10.0 Ulemavu

Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inatafsiri ulemavu kuwa ni hali ya mtu kupoteza au kupungukiwa na fursa ya kushiriki katika maisha ya kawaida ya jamii kwa kiwango sawa na watu wengine kutokana na sababu za kimwili, kiakili au kijamii. Takwimu za hali ya ulemavu ni muhimu kwa ufuatiliaji wa kiwango cha utendaji kazi wa idadi ya watu na ni muhimu pia kwa ufuatiliaji wa ubora na matokeo ya sera na programu mbalimbali za kitaifa, tathmini ya mahitaji, kuendeleza na kulinda haki za watu wenye ulemavu.

**Matokeo Muhimu**

i. Kiwango cha ulemavu kwa watu wenye umri wa miaka 7 na kuendelea Tanzania ni asilimia 11.2;
ii. Karibia asilimia 58 ya watu wenye ulemavu waliripoti kuwa maradhi ni sababu kuu ya ulemavu wao; na
iii. Karibia asilimia saba (7) ya watu wenye ulemavu waliripoti kuwa ajali ni sababu ya ulemavu wao.

Watu wenye ulemavu wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kupata huduma muhimu za kijamii kama vile elimu, afya, ufikiaji na utumiaji wa majengo kwa urahisi na fursa za kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Aidha, baadhi ya watu wenye ulemavu wanapitia hali zisizoridhisha kama kutokujikubali, unyanyapaa, ubaguzi, umaskini na kutengwa katika jamii.

**Tafsiri ya Kisera**

i. Kuongezeka kwa idadi ya watu wenye ulemavu kunaweza kuongeza gharama za matunzo katika kaya na jamii na kusababisha matokeo mabaya ya kijamii na kiuchumi kama vile umaskini unaotokana na kukosa fursa muhimu, mfano elimu, ajira na upatikanaji wa kipato; na
ii. Watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi yaliyopo hatarini zaidi katika jamii na hivyo, rasilimali zaidi zinahitajika ili kuwasaidia.

**Mapendekezo ya hatua za Kisera**

i. Serikali na wadau wengine kutenga rasilimali zaidi ili kuhakikisha ustawi wa watu wenye ulemavu unazingatiwa;
ii. Serikali na wadau wengine kuongeza ruzuku na misaada kwa watu wenye ulemavu, na wale wanaowatunza au kuishi na watu wenye ulemavu;
iii. Serikali na wadau wengine kuhakikisha kuwa wanaweka mazingira mazuri ya watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za maendeleo yao binafsi na ya taifa; na
iv. Serikali na wadau wengine kuimarisha programu za afya na usalama ili kupunguza matukio ya maradhi na ajali ambavyo vimeonekana kuwa ni vyanzo vikuu vya ulemavu nchini.

## 11.0 Nishati

Nishati ni moja ya maeneo ya kipaumbele kwa Serikali katika kuboresha afya na ubora wa maisha ya Watanzania. Serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 ambayo inalenga kuimarisha utoaji wa huduma bora za nishati kwa bei nafuu na endelevu.

**Matokeo Muhimu**

i. Karibia asilimia 56 ya kaya zinatumia kuni na asilimia 25.9 zinatumia mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia;
ii. Asilimia 16.0 ya kaya zinatumia nishati safi kwa ajili ya kupikia;
iii. Asilimia 37.4 ya kaya zinatumia umeme kutoka gridi ya Taifa kwa kuangazia; na
iv. Asilimia 32.4 ya kaya zinatumia umeme wa jua kwa kuangazia.

**Tafsiri ya Kisera**

i. Kuendelea kutumia kuni na mkaa kama vyanzo vikuu vya nishati ya kupikia kunasababisha uharibifu wa mazingira kwa kukata miti, kuharibu udongo na kutoa gesi ukaa ambavyo vina athari kwenye bioanwai, mabadiliko ya tabia nchi na uendelevu wa muda mrefu wa maliasili;
ii. Matumizi ya kuni na mkaa kwa kupikia husababisha uchafuzi wa hewa ndani ya nyumba ambayo inahusishwa na hatari kubwa ya magonjwa ya kupumua na matatizo mengine ya kiafya; na
iii. Kuongezeka kwa matumizi ya umeme na vyanzo vingine vya nishati safi, kunaweza kusababisha kupungua kwa uharibifu wa mazingira. Hii inaonesha kuwa mafanikio yameanza kupatikana katika matumizi ya nishati safi.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali na wadau wengine wazingatie kutoa motisha na kushawishi matumizi ya nishati mbadala ya kupikia na kuangazia kwa kupunguza kodi ili kushusha gharama za nishati safi;

ii. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine kusaidia upatikanaji wa miundombinu ya bei nafuu ya kuweka na kuunganisha nishati safi; na

iii. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine kutoa elimu ya nishati mbadala na ushawishi wa kutumia teknolojia yenye ufanisi wa nishati.

## 12.0 Umiliki wa Ardhi

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Umiliki ardhi huleta tija na ufanisi katika shughuli za maendeleo. Ardhi ni rasilimali ambayo thamani yake huongezeka kila wakati hivyo umiliki wa ardhi wenye nyaraka za kisheria humpa mmiliki usalama wa ardhi yake.

**Matokeo Muhimu**

i. Karibia nusu (asilimia 47.2) ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanamiliki ardhi bila kuwa na nyaraka za kisheria; na

ii. Asilimia 10.6 ya wanawake Tanzania wanamiliki ardhi peke yao ikilinganishwa na asilimia 18.1 ya wanaume.

**Tafsiri ya Kisera**

Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Ardhi ni kukuza na kuhakikisha mfumo salama wa umiliki wa ardhi, kushawishi matumizi endelevu ya rasilimali za ardhi, na kuwezesha maendeleo mapana ya kijamii na kiuchumi bila kuvuruga au kuhatarisha uwiano wa ekolojia ya mazingira. Usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi ni suala muhimu la kisera kwa Tanzania.

i. Umiliki wa ardhi wenye nyaraka za kisheria unampa mmiliki usalama wa ardhi yake;

ii. Mila zinazobagua na kukuza usawa wa jinsia katika umiliki wa ardhi zinaweza kusababisha umiliki wa ardhi usio na usawa kijinsia; na
iii. Wanawake wanaomiliki ardhi wanaweza kujihusisha na shughuli za kuzalisha kipato hivyo kuwawezesha kiuchumi, kupunguza umasikini na maisha bora kwa wote.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali na wadau wengine kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera ya ardhi (1997) kwa lengo la kuhakikisha mchakato wa umiliki wa ardhi kwa kujenga uwezo wa idara husika;
ii. Serikali kuweka utaratibu wa kushughulikia utofauti wa kijinsia wa umiliki wa ardhi katika maeneo husika na kulinda makundi maalumu katika umiliki wa ardhi;
iii. Serikali kuimarisha vifungu vya kisheria kwa kuviweka sambamba na haki za kikatiba ili kuwa na usawa katika mchakato wa ugawaji wa ardhi kwa wanawake na wanaume;
iv. Serikali na wadau wengine wahamasishe na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za wanawake katika umiliki wa ardhi na faida za umiliki wa pamoja ili kukuza usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu na kupunguza umasikini; na
v. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kuongeza kasi ya kutoa nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi.

## 13.0 Maji na Usafi wa Mazingira

Upungufu wa maji ya kutosha na usafi wa mazingira vinaweza kuwa na athari mbaya kwa afya ya binadamu na ustawi. Hali hii inaweza kuhusishwa na maambukizi ya magonjwa kama vile kuhara, kipindupindu na homa ya matumbo. Umoja wa Mataifa unatambua upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kuwa ni haki ya msingi ya binadamu.

**Matokeo Muhimu**

i. Karibia asilimia 70 ya kaya hutumia maji ya kunywa kutoka vyanzo vilivyoboreshwa;
ii. Karibu asilimia 91 na 56 ya kaya binafsi katika maeneo ya mjini na vijijini mtawalia hutumia maji ya kunywa kutoka vyanzo vilivyoboreshwa;
iii. Karibu asilimia 60 ya kaya hutumia vyoo vilivyoboreshwa;
iv. Karibu asilimia 41 ya kaya za watu katika maeneo ya vijijini hutumia vyoo vilivyoboreshwa; na
v. Karibu asilimia 9 ya kaya katika maeneo ya vijijini hazina vyoo.

**Tafsiri ya Sera**

i. Kaya nyingi za mjini (91%) zinatumia maji kutoka kwenye vyanzo vya maji vilivyoboreshwa. Hata hivyo, asilimia 56 ya kaya za vijijini zinazotumia maji kutoka kwenye vyanzo vilivyoboreshwa ni chini ya lengo la kitaifa la kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025/26;
ii. Asilimia 40 ya kaya zote nchini bado zinatumia vyoo visivyoboreshwa au hazina vyoo kabisa. Hii inaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu, kuhara pamoja na uchafuzi wa mazingira; na
iii. Karibu asilimia 41 ya kaya za vijijini zinatumia vyoo vilivyoboreshwa. Hii ni chini ya lengo la kitaifa la kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2025/26.

**Mapendekezo ya Sera**

i. Serikali iendeleze juhudi za kuboresha upatikanaji wa maji kutoka vyanzo vilivyoboreshwa kwa kuweka mkazo zaidi vijijini ambapo idadi kubwa ya kaya bado zinatumia maji kutoka vyanzo visivyoboreshwa;
ii. Serikali na wadau wengine kuimarisha kampeni zinazoendelea kuhusu athari zinazoweza kutokea kwa kutotumia vyoo vilivyoboreshwa; na
iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zilizopo ambazo zinahitaji kila kaya kuwa na vyoo bora.

## 14.0 Upatikanaji na Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imeongeza kasi ya maendeleo kijamii na kiuchumi duniani. Nchi zimeweka kipaumbele katika uwekezaji wa mfumo wa ikolojia ya kidigiti ili kubadilisha na kuboresha uchumi wao. Kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya TEHAMA katika kuwezesha na kuharakisha maendeleo kwa jumla. Upatikanaji na matumizi ya takwimu bora za TEHAMA zina athari chanya kwa uchumi na jamii kwa ujumla

**Matokeo muhimu**

i. Takribani asilimia 19 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanamiliki simujanja au vishikwambi;
ii. Asilimia 21 ya wanaume wanamiliki simujanja au vishikwambi ambapo kwa wanawake ni asilimia 17 ;
iii. Takribani asilimia 34 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanaoishi mjini wanamiliki simu au vishikwambi ambapo kwa maeneo ya vijijini ni asilimia 9 tu ;
iv. Umiliki wa ngamizi (computer) ni chini ya asilimia 4 ikilinganishwa na asilimia 19 ya umiliki wa simujanja au vishikwambi; na
v. Takribani asilimia 37 ya kaya nchini Tanzania zinamiliki mwengoya (radio) na asilimia 27 zinamiliki runinga.

**Matokeo ya Sera**

i. Kiwango cha kupatikana kwa huduma ya TEHAMA kati ya kaya na watu binafsi inaonyesha kuwa, sekta hiyo inakua katika mwelekeo sahihi. Licha ya ukuaji huu, ushahidi kutoka kwenye Sensa ya Watu na Makazi, (SWM, 2022) na taarifa za kiutawala inaonyesha kuwa pengo la mgawanyo wa dijiti bado ni mkubwa. Kwa mfano, katika mtandao wa asilimia 72 ya kihamisha-data kasi (broadband), iliyotengwa kwa Tanzania, ni asilimia 45 tu inayotumika.

ii. Umiliki na matumizi ya vifaa vya TEHAMA (simu janja, vishikwambi na ngamiza) ni wa chini sana, hivyo hupunguza matumizi ya huduma ya kihamisha –data kasi;
iii. Upatikanaji na matumizi ya huduma ya TEHAMA ni mdogo miongoni mwa wanawake ikilinganishwa na wanaume katika maeneo ya mjini na vijijini; na
iv. Umiliki na matumizi hafifu ya mwengoya na runinga hudunisha mawasiliano ya habari na huduma muhimu.

**Mapendekezo ya Hatua za Kisera**

i. Serikali iboreshe upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA vya bei nafuu kwa kupunguza kodi na kuanzisha programu za kusoma na kuandika kidijiti katika mtaala wa elimu ili kuziba pengo la mgawanyiko wa **vifaa vya kidijiti**. *Serikali na sekta binafsi* wanapaswa kukuza matumizi ya vifaa vya kisasa vya TEHAMA kupitia elimu ya kidijiti, upatikanaji wa huduma himilivu, upatikanaji wa maudhui ya mtandaoni na vifurushi;
ii. Serikali ifikirie kukuza upatikanaji na ujuzi katika teknolojia ya kidijiti na kuanzisha miradi ya ufadhili ili kukabiliana na upatikanaji mdogo na matumizi ya huduma ya TEHAMA miongoni mwa wanawake na makundi yaliyotengwa (watu wenye ulemavu, vijana, watoto, wazee na watu wanaoishi katika maeneo ya mbali); na
iii. Serikali ifikirie kufanya tafiti za umiliki na matumizi ya TEHAMA kwenye kaya ili kubaini kiasi cha matumizi ya TEHAMA ambayo hayakujumuishwa kwenye Sensa